# *MARIA MTAKATIFU*




2. Ulizaliwa safi, ee mtoto wa Mungu. Dunia haimwoni mwingine kama wee.
Milele Mungu Mkuu amekubariki, kuliko wanawake katika Mwanao.

3. Malkia mwenye taji, la nyota kichwani. Bushuti lako jua na mwezi miguuni.
Milele Mungu mkuu amekuagiza, kumshinda joka mbaya, ee Mama bila waa.

3. Mama safi wa moyo, utupatie shimeyo. Utupeleke mbinguni tukamwone Mwanao.
Milele Mungu Mkuu, amekuteua, Bikira Mtakatifu na Mama mtukufu.

4. Tunakushangilia, na sisi wanao. Heshima zetu pokea, tu wana wajao.
Milele Mungu Mkuu, amekuteua, Bikira mtakatifu na Mama Mtukufu.